TAMTHILIA: KITHAKA WA MBERIA: KIFO KISIMANI

1. " Nafurahi kusikia unawaza kuhusu umma"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili

(Alama 4)

(b) Thibitisha kauli hii kwa kuonyesha nafasi ya vijana katika kutetea haki za jamii.

(Alama 16)

HADITHI FUPI: K. W. WAMITILA
MAYAI WAZIRI WA MARADHI

Jibu swali la 2 au la 3

2. "Mwanamke ni adui ya nafsi yake mwenyewe." Thibitisha dai hili kwa kuzingatia hadithi mbili,

"Uteuzi wa Moyoni" na "Ngome ya nafsi".

(Alama 20)

NDIMI ZA MAUTI. TIMOTHY M. AREGE.

3. " Alikiuma kidomo chake na kuchukua hatua ya mwisho. Moyoni alihisi ndimi za aina yake zikimwunguza. Ndimi za mauti."

(a) Fafanua muktadha huu.

(Alama 4)

(b) Kwa kutolea mifano fafanua aina zozote mbili za ndimi kulingana na hadithi hii.

(Alama 4)

(c) Ni sababu gani zilizochangia mkasa huu kufikia kiwango ulichofikia.

(Alama 4)

(d) Fafanua majuto kwa kila mtekelezi wa mkasa huu

(Alama 8)

5 FASIHI SIMULIZI

(a) Tofautisha baina ya ulumbi na soga

(Alama 4)

(b) Fafanua sifa za ulumbi

(Alama 7)

(c) Taja baadhi ya Miviga maarufu katika jamii za Afrika.

(Alama 3)

(d) Eleza umuhimu wa Miviga katika jamii

(Alama 6)

USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7

6. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata***.

HISIA

Ewe hisia!
Umeniamshia ndoto niloisahau zamani
Umelimsha mwangu moyoni
nyimbo ya kale
na mdundo usomvutia
ila hayawani wa mwangu rohoni.

Tulia sasa tulia.
Hebu tulia ewe hisia ulo mtimani.
Nakataa katu kusisimka
kwa sauti yako laini
Kwani njia zetu ni panda
daima hazioani

Umesubutu vipi kuniita
kutoka mwako ngomeni
ulimosahauliwa tangu zamani
Basi yawache maombolezi yako yaso maoni,
yawateke hao mashujaa wa kale
watu walo kaburini.

Hebu tulia, usiniingilie
usinihangaishe!
Kukuandama katu haimkini
Kwani hata sasa…. kwa kukuwaza tu dakika hini
naona majuto ya mbali moyoni
kama kwamba nimegawa wangu wakati
na wazimu, majinuni.
Basi nenda zako hisia…shuu… hebu tokomea.

(a) Huu ni utungo wa aina gani?

(Alama 2)

(b) Kwa kutoa mifano fafanua sifa zinazoufanya utungo huu kuwa shairi.

(Alama 4)

(c) Eleza mawazo ya mshairi katika shairi hili

(Alama 5)

(d) Taja na ueleze mbinu tatu za kifasihi katika shairi hili.
(Alama 6)
(e) Andika maneno yafuatayo kwa lugha sanifu
(Alama 3)

(i) Niloisahau
(ii) Umesubutu
(iii) Mtimani

USHAIRI

7. ***<u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuatia.</u>***

Sikimbii, Siogopi, hali yangu nachelea.
Sivijui, visa vipi, pale nyuma kutokea
Niendako, sikujui, mkimbizi ninaitwa!

Sitoroki, nchini mwangu, ugenini kutamani
Sidiriki, malimwengu, yananizonga jamani
Niendako, sikijui, usalama nazengea!

Siyajui, nisemayo, machafuzi nayapisha
Siyajui, nionayo, ni maasi ya kutisha
Niendako, sikujui, amani najitakia

Sipotei, sipumbai, hali njema naisaka
Sishangai, sitambui, chanzo cha yangu mashaka
Niendako, sikujui, maskani natafuta.

Afrika, Afrika, wana wako tunalia
Twateseka, twateseka, bara letu kulilia
Kwa majanga, na visanga, ukimbizi kuzidisha.

Viongozi, viongozi, mwongozao Afrika
Mumaizi mumaizi, utulivu kuuweka
Zi nchi zetu, ukimbizi kupunguza.

(a) Lipe kichwa mwafaka shairi hili
(Alama 1)
(b) mikondo mitatu ya shairi hili.
(Alama 3)

(c) Onyesha mpangilio wa mizani na vina katika ubeti wa tano
(Alama 4)

(d) Mshairi ana ushauri gani kwa viongozi wa kiafrika?
(Alama 2)

(e) Mshairi ana falsafa gani?
(Alama 2)

(f) Taja na ueleze tamathali zozote mbili katika shairi hili
(Alama 4)

(g) Shairi la aina hii hutumiwa vipi katika Fasihi simulizi
(Alama 2)

(h) Eleza maana ya msamiati huu kwa mujibu wa shairi
(Alama 2)

(i) Sidiriki

(ii) Nazengea